# HALMASHAURI YA WILAYA YA NZEGA

SHULE YA SEKONDARI MABONDE,

S.L.P 174,

**BUKENE – NZEGA.**

TAREHE__________________

KUMB.NA. MBSS/JI/VOL I/2021

JINA LA MWANAFUNZI____________________________________

SHULE YA MSINGI ALIYOTOKA______________________________

S.L.P________________________

**YAH: <u>MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MABONDE WILAYA YA NZEGA MKOA WA TABORA MWAKA 2021</u>**

**1. UTANGULIZI**

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021, Shule ya Sekondari Mabonde ipo umbali wa kilometa moja kutoka katika kijiji cha Kahamanhalanga Shule ilipo. Tumia usafiri wa baskeli kufika shuleni muhula wa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 11/01/2021. Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 11/01/2021 saa moja kamilihadi saa nane na nusu za mchana. Mwisho wa kuripoti shuleni ni tarehe 22/01/2021 ndani ya siku (14) kumi na nne.

**2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

2.1. Sare za shule

(a) Rangi ya sareya shule hii ni kijani jeshi wavulana suruali na tai yake wasichana sketi ndefu na skafu yake. Mashati meupe yenye mikono mirefu, sweta shingo muundo wa V mbele rangi ya kijani jeshi na tisheti za kola rangi ya kijani yenye nembo mgongoni na kifuani kushoto, soksi nyeupe waschana na nyeusi wavulana

(b) Vazi la hijabu suruali isiyobana kijani jeshi na blauzi nyeupe inayovuka makalio yenye mikono mirefu

(c) Sare ya michezo wavulana bukta nyekundu wasichana bukta ndefu inayovuka magoti rangi ya bluu.

NB: Sare zote mzazi atamgharamia mwanaye.

2.2 Daftari,9 Kalamu za wino bluu au nyeusi,penseli na Mkebe wa seti za hesabu.

## 3.0 Sheria na kanuni muhimu za shule hii

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu na 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa sheria na 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya elimu sayansi na technolojia ,yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya RAIS TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

a) Heshima kwa viongozi, wazazi,wafanyakazi wote,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima;
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima;
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation);
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazo pewa;
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na
i) Kutunza mali za Umma.

## 3.1 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa Shule.

a)Wizi
b) Uasherati na Ushoga
c) Ubakaji.
d)Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi,cocaine,mirungi,kubeli na kadhalika.
e) Kupigana au kupiga.
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
g) Kudharau Bendera ya Taifa.

h) Kuwa mjamzito /kupata mimba.
i) kuoa au kuolewa
j)Kutoa mimba.
k)Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
l)Kukataa adhabu kwa makusudi.
m)Kuwa na simu ya mkononi

**MAKOSA MENGINE NI.**

(i) Kuwa mvivu darasani na nje ya darasa,hii ni pamoja na kutokufanya mazoezi au mitihani na kutoshiriki kazi za nje.
(ii) Kusema uongo
(iii) Kuwa mtoro au mchelewaji
(iv) Kupiga kelele darasani
(v) Kupatikana na makosa ya jinai

**ADHABU ZIFUATAZO ZINAWEZA KUTOLEWA SHULENI**

a) kuchapwa viboko visivyozidi sita kwa wakati mmoja makalioni(wavulana) kwa kulala chini na mikononi (wasichana) kwa kunyoosha mkono.
b) Kufanya kazi ngumu mfano' kuchimba shimo la taka au kung'oa visiki
c) Kupewa onyo la maandishi
d) Kusimamishwa shule kwa muda
e) Kufidia gharama za uharibifu
f) Kufukuzwa shule

**4.0 Mambo Mengine Muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi.**

a) Medical Examination Form(fomu ya daktari) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali.Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shuleni.

b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.

c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria,kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

**5.0 Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

.......................................................

**MKUU WA SHULE**

**SIMU NAMBA** 0684-736300

**GOVERNMENT OF TANZANIA**
**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

FROM THE HEADMISTRESS,
MABONDE SECONDARY SCHOOL,
P.O. BOX 174,
**NZEGA.**

**TO THE MEDICAL OFFICER**

______________________________
______________________________
______________________________

**REF:** ____________________________________________

**NAME OF STUDENT:** ____________________________________________

Please examine the above named student as to his/ her physical and mental fitness for a full time student of this school. The examination should include the following categories.

a. Eye – sight ..........................................................................
b. Hearing ..........................................................................
c. Speech ..........................................................................
d. Limbs ..........................................................................
e. Veneral Diseases ..........................................................................
f. Leprosy ..........................................................................
g. Peptic ulcers . ..........................................................................
h. Epilepsy ..........................................................................
i. Tuberculosis . ..........................................................................
j. Neurosis ..........................................................................
k. Pregnancy ..........................................................................
l. Other diseases ..........................................................................

**PART B: CERTIFICATE.** (To be completed by a government medical officers )

I have examined the above named student and consider that she/ he is physically and mentally fit/ unfit

**Name** .............................................. **Signature** .................. **Date** ..............

**KIAMBATANISHO A**

**FOMU YA MZAZI KUKIRI KUTEKELEZA MAAGIZO YOTE.**

Mimi ________________________________________Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi ________________________________________ninakubaliana na sheria zote za shule kanuni na maelezo yatakayotolewa na shule pia naahidi kushirikana na shule katika kumsaidia mtoto wangu kitaaluma na hasa kuhakikisha, anahudhuria shuleni kila siku.

________________________ ________________________

**Sahihi ya Mzazi /Mlezi** **Tarehe**

**KIAMBATANISHO B**

**KIAPO CHA MWANAFUNZI**

Mimi ________________________________Mwanafunzi wa shule ya Sekondari ______________ naapa kwamba nitatii sheria zote za shule kwa muda wote nitakaokuwa nasoma shuleni hapa,pia sitashiriki mgomo wa aina yoyote wala kufanya fujo shuleni wala makosa yoyote ya jinai.Endapo nitakwenda kinyume basi hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yangu.

Aidha naapa vilevile kwamba nitajibidisha katika masomo ,kwa nguvu na uwezo wangu wote.Hivyo nitahudhuria vipindi vyote darasani na nje ya darasa kulingana na ratiba ya shule.

Naahidi vilevile kwamba nitakuwa mstari wa mbele kuyatunza na kuyaboresha mazingira ya shule yangu nakwamba mimi mwenyewe nitakuwa msafi daima.Nitakapoharibu mali yoyote ya shule nafahamu nitawajibika kulipa.

Kinyume na utaratibu hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yangu.

________________________ ________________________

**Sahihi ya Mwanafunzi** **Tarehe**